

MWONGOZO WA KARATASI YA KWANZA

1. Kuandika Memo.

Mtahiniwa ajikite katika mambo yafuatayo:

Muundo

Sura iwe ya memo.

Kichwa

Kichwa kionyeshe kuwa ni memo

Kutoka kwa

Kwenda kwa

Tarehe

Mada/kiini

Mwili

Mtahiniwa ataje usuli wa mada memo.

Mathalan; **kumekuwa na visa vingi vya utovu wa nidhamu...**

Maoni – kuhusu visa vya utovu wa nidhamu mwingoni mwa wanafunzi

- Matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanafunzi
- Wizi wa mitihani
- Kupigana shuleni
- Kurudia chakula katika bwalo
- Kutowaheshimu viranja
- Kuchelewa darasani
- Kuchelewa kufika shuleni baada ya likizo
- Kupiga kelele darasani
- Wizi wa vitabu n.k

Hatua zitakazochukuliwa

- Kutumwa nyumbani waje na wazazi
- Kupewa ushauri nasaha kuhusu madhara ya daa za kulevya
- Kupimwa kwa wanafuzi kuhakikisha hawatumii dawa za kulevya
- Kuwatuma kwa daktari wa kiakili
- Wezi wa mitihani kurudia kufanya mitihani hiyo
- Wezi wa vitabu kununua vitabu maradufu

- Kupiga kelele darasani, wanafunzi wapewe kazi ya kufanya kuwaadhibu
- Kurudia chakula –wataosha bwalo mara mbili kwa wiki
- Kuchelewa kufika shuleni- mwanafunzi arudi na mzazi n.k

Hitimisho

- Sahihi
- Jina
- Cheo

2. Kuandika tahariri.

Mtahiniwa ajikite katika mambo yafuatayo:

Muundo

Sura iwe ya tahariri.

Kichwa

Kichwa kionyeshe kuwa ni Tahariri ya gazeti la Wosia.

Mahali

Tarehe

Wakati

Anwani iwe moja, ile ya Gazeti la Wosia.

Mwili

Mtahiniwa ataje usuli wa mada ya tahariri.

Umuhimu wa mitandao ya kijamii

Baadhi ya hoja ni kama;

- Mitandao imesaidia katika mafunzo na utafiti wa kielimu wa mtandaoni
- Burudani
- Kuwaunganisha wasomi kutoka mataifa mbali mbali
- Matangazo ya biashara
- Urahisi wa kupata habari
- Kuunganisha jamii
- Kupunguza gharama za kuandaa mikutano
- Kulipa kutumia simu na kupunguza matumizi ya pesa hai
- Kununua na kuuza bidhaa miitandaoni kwa mfano Jumia, kilimall n.k
- Huduma za benki za mitandao n.k

Hitimisho

- Msimamo wa gazeti utolewa hapa
- Idhibati
- Jina
- Cheo

3. Mpanda ngazi hushuka

Hii ni insha ya methali

Mwanafunzi aandike kisa kitakachoafiki methali hii.

Maelezo ya methali:

Mhusika alipanda ngazi mathalani kupata cheo au kazi. Sehemu ya pili mhusika akafutwa au kuachishwa kazi.

Kisa kiwe na sehemu mbili mathalan, kupanda ngazi na sehemu ya kushuka.

Kisa kioane na maelezo ya methali hii.

Baadhi ya visa.

- Mhusika aliyepata kazi baadaye akafutwa
- Mhusika, biashara yake ilinawiri baadaye ikaporomoka.
- Mchezaji aliyevuma baadaye akaporomoka n.k

4. Insha ya mdokezo

Hii ni insha ya mdokezo. Mwanafunzi aandike insha itakayoanza kwa mameno aliyopewa.

Baadhi ya visa;

- Mhusika aliyekubwa na shida fulani kisha akabahatika kupata mdhamini
- Mwanafunzi aliyekumbwa na ugumu wa maisha shuleni kulipa karo kisha akapata mdhamini
- Mwanafunzi aliyepata shida na somo fulani hadi alipopata rafiki aliyewekeza n.k

Tanbihi ya usahihishaji.

- Mtahiniwa akikosea sura ya insha akadiriwe ila aondolewe **4S**
- Akikosa anwani asiadhibiwe- anwani sio lazima.
- Hoja zilenge mada
- Katika swali la kwanza, hatua zitakazochukuliwa zitolewe (huu ndio mtego)
- Hakikisha kwamba urefu wa insha unazingatiwa (kadiria)

- Insha ya methali iwe na pande mbili.
- Tusome kazi za wanafunzi tafadhali. Tusipeane BAKISHISHI bila kusoma na kuandika udhaifu huo kwa karatasi ya mwanafunzi.
- Iwapo ni lazima BAKISHISHI ni alama **03/20**

Visit www.freeksepastpapers.com to access more content